JUA

GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi : *Mutiri-wa-Bashara*

Mwaka wa 18 toleo la 397


# Arkidiosezi ya Bukavu na viongozi wa jimbo, wafia nini ?

Mjini Bukavu, wakaaji wapigwa bumbuazi kutokana na mzozo ulioko kati ya arkidiosezi katoliki na viongozi pia wakuu wa serkali jimboni. Kisa cha mzozo huo ni kiasi cha udongo chenyi hektari 6 na vipande ambako nyumba 9 zimekwisha kujengwa na zingine 5 zatezamiwa kumalizika kujengwa baadae. Majengo hayo yafanyika mkoani Karhale ya pili mtaani Kadutu kwa manufaa ya kituo cha vilema "Heri Kwetu". Lakini kazi za ujenzi kasimamishwa na hatua kachukuliwa na kamati ya Chama "MPR" jimboni mwa Kivu ya Kusini.

**Kwa nini ?**

Akiwahubiria wahuzuriaji katika misa kasomwa kwa ajili ya roho ya marehemu Mama Mobutu, mke wa kwanza wa Raïs wa Jamhuri ya Zaïre na ambaye kafariki dunia tangu miaka 12 sasa, Mosinyori Mitima-Eluga-Omu-Nda, padri mkuu wa parokia katoliki ya Ibanda, Mama wa Amani, kanena kuwa

Ufuat. pa uk.12

# Mwaka wa 1989 kwa ufupi

**Katika mwezi wa :**

**JANUARI:Masilizano kuhusu urafiki kati ya Ufalme wa Ubelgigi na Jamhuri ya Zaïre kajulishwa**

1:Prezidenti - muundaji wa Chama cha Mapinduzi"MPR", Mareshali Mobutu kawasiri mjini Mbuji-Mayi ambako kasherehekea sikukuu ya mwaka mpya.

4 : Kumbukumbu la sikukuu ya Mashahidi wa Uhuru nchini Zaïre.

6:Mfalme Hiro-Hito wa Ujapani kafariki dunia

9:Wanamemba wa Kamati kuu ya Chama "MPR" kakutana.

10:Askari jeshi wa Cuba katoka nchi ya Angola na kurudi makwao

26:Nchini kaundwa Baraza imara la shauri na maoni kuhusu maendeleo (CCPD)

28:Mvua kali kararua nyumba yapata 300 mjini Uvira

**FEBRUARI:Univasti ya Kinshasa kafungwa**

2:Raïs Pieter Botha wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini kajiuzulu

15 : Kutokana na mgogoro katukia kunako univasti na mashule makuu 4 haya kafungwa

24 : Raïs Mobutu wa Zaïre kahuzuria majishi ya mfalme Hiro-Hito nchini Ujapani. Mfalme mpya aitwa Aki Hito

24-28:Askofu Desmondo Tutu wa Kanisa la kianglikani nchini Afrika ya Kusini kawasiri nchini Zaïre katika ziara ya kutangaza neno la Mungu

**MARSI:Mishahara ya wafanyakazi wa serkali kaongezwa**

6:
Baraza la imara la shauri na maoni kakutana kwa mara ya kwanza mjini Gbadolite

20:Univasti ya Kinshasa kafungua tena milango yake. Sikukuu ya nchi zinazosema na kuandika lugha la kifransa

24:Mwami Ntambuka N'Sibula Kabego II wa Idjwi kafariki dunia. Mkombozi ni Ntambuka Balekage Mihigo II

30:Mtaguso usio wa kawaida kafanywa na Muungano waandishi na wapasha habari mjini Kinshasa. Mwananchi Mutiri-wa-Bashara, prezidenti wa muungano huo kagombolewa na mwananchi Kitutu Oleontwa

28:Kutokana na mmomonyoko wa udongo, watu 148 kafikilia kukosa makao. Kwani nyumba kalazwa bila huruma na hali hiyo.

**APRILI: Mlima wa moto Nyamulagira katomboka**

22:Jimboni mwa Ki-

Ufuat. pa uk.14

## Uhariri

### Heri na Fanaka

Kweli, mwaka 1989 katezamiwa kupita kama umeme angani. Wote walio bado duniani twafurahia na kuukaribisha mwaka mpya 1990 tukimshangilia Mweny'Ezi, Baba Mungu Muumbaji, kwa vigelegele.

Tukitupa jicho mwakani 1989,ndugu, marafiki, majirani, sisi wenyewe,labda, na wengineo kazaa wa kazaa kalazwa na matatizo mbalimbali. Lakini tukichungua kwa kiini-macho mwaka huo wa 1989 umepita kama upepeo na kufyatuka kama swala.

Mwakani humo, magumu mengi katuangamiza kama vile mauaji, wizi, njaa, magonjwa na kazalika. Na mengi kati ya hayo yote yaliweza kugunduliwa, kupashwa katika nakała za gazeti lenu tukufu ao kusikilika kwa wenzio.

Nchini mwetu Zaïre viongozi, wakuu na raïa wakiungana mkono Chama-serkalini walihusika na uhusiano wapaswa kuweko kati ya nchi jirani pia rafiki, afia ummani, mimomonyoko ya arzi na uharibifu wa mabarabara kutokana na maji ya mvua na hata kuwatia jamaa kazaa katika vilio na mengineo magumu na mambo mengi kuangamiza raïa.

Ulimwenguni, wataalam nchini Ujapani kahakikisha kuwa wamegundua dawa muhimu na iliyo bora kwa kuulaza ugonjwa haramu wa SIDA baada ya mganga mtaalam Mwana-Zaïre, daktari Lurhuma, kugundua dawa ya kulaza viini (mikrobi) vimoja vya ugonjwa huo. Na ambao waangamiza watu wengi duniani siku za leo, wake kama vile waume.

Barani Afrika, serkali kazaa kapindulíwa, wakuu kutiwa nguvuni, kuuwawa na wengineo kutoka gorogoni ama kukimbia hadi nchi za kigeni kutokana na siasa yao. Namibia huru yatezamiwa kuongozwa na bwana Sam Nujoma ambaye kachaguliwa kama vile raïs wa kwanza akiungwa mkono na wafuasi wa chama chake cha ukombozi Swapo, masikilizano kafanyika kati ya ndugu adui wa Angola Eduardo dos Santos, Jonas Savimbi toka siasa ya amani kaendeshwa na Mareshali Mobutu Barani Afrika, mzozo wa Sudania, Mauritania, Ethiopia na penginepo.

Barani Azia, vita vikali vyaendelea kati ya wananchi wa Libania hivyo kati ya waumini wa dini mbalimbali nchini India, Iran, Irak, Afghanistan, mapinduzi kafanywa Urusi na zingineo nchi. Kati ya mambo hayo, mengi yalionya utumizi wa silaha wa vinginevyo vifaa vya vita kisasa.

Wakati huyo, Ulaya imetikisika katika upande wa mashariki. Pepo ya bwana Gorbatchev, raïs wa Urusi imeambukia nchini nyingi za kisosialisti kama vile Roumania, Yougoslavia, Bulgaria na Ujerumani zote mbili. Ni hivi ule mkuta wa Berlin uitwao ukuta wa haya umefunguka na utezamiwa kuangushwa pamoja na kikomunisti ukiacha watu huru, wakivuta hewa ya kidemokrasia.

Ebu ! Gazeti lako tukufu "JUA" ingawa magumu mengi laingia katika mwaka wake wa 18 sasa. Kiongozi-mhariri, mwananchi Mutiri-wa-Bashara, waandishi na watumishi wake wote kajitatanua, ginsi waliwezavyo, kuwajulisha yote yaliyopita. Toka hapo, hawa wawatakia wasomaji wake popote walipo mwaka mwema, wa heri na fanaka na wa maendeleo.

Bisimwa L-B. Tserou